BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 25 Februari, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Itasomwa

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Tume na Hali ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Nchini kwa Mwaka 2023/2024.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Tume na Hali ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Nchini kwa Mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

8. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

   Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa wanawake wenye ulemavu wanapata elimu, afya na ajira bila ya vikwazo.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

157. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

   Licha ya Serikali kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi, wapo baadhi ya watendaji hawana utaratibu mzuri wa utoaji wa huduma kwa wateja (Customer Care).

   (a) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha watendaji wa Serikali wanajengewa uwezo katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

   (b) Kwa nini Serikali haijaamua kwamba suala la upimaji wa kutoa huduma kwa wananchi (Service Delivery Performance Measurement), likawa ni kipimo cha utendaji kazi wa watumishi wake.

### Wizara ya Fedha na Mipango:

114. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

   Kwa sasa Serikali inakusanya mapato na kufanya matumizi yake kupitia mifumo mbalimbali kwa lengo la kudhibiti upotevu na matumizi mabaya.

   (a) Je, mifumo ya kutambua wageni wanaoingia na kutoka mahotelini imeshaunganishwa.

   (b) Je, ni hoteli ngapi zimeshaunganishwa kwenye mfumo, ili kutambua wageni wanaoingia na kutoka kila siku.

237. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa kuwa kumekuwa na makusanyo ya fedha za kuongeza ujuzi (SDL) kutoka kwa waajiri ambazo zinatumika katika kuendeleza wanafunzi kuongeza ujuzi wao. Na kwa kuwa fedha hizo zinakusanywa na Mamlaka za Mapato kwa ajili ya kutumika kama sheria inavyoelekeza.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha za SDL kimekusanywa katika mwaka wa fedha uliopita 2024/2025 na mwaka huu mpaka sasa zimekusanywa kiasi gani.

(b) Je, mgawanyo wa fedha hizo uko vipi kwa vyuo vya amali na skuli za ufundi.

## <u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

80. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Skuli ya Dkt. Salim Ahmed Salim ni miongoni mwa skuli zinazopokea wanafunzi wa michepuo kutoka skuli mbalimbali za Pemba. Na kwa kuwa skuli hii ipo kando kidogo ya mji, hali inayopelekea usumbufu wa makaazi ya wanafunzi hao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga dahalia katika skuli hii, ili kuwaondoshea usumbufu wanafunzi husika.

147. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa suala la elimu ya kuyahifadhi, kuyalinda pamoja na kuyatunza mazingira yaliyotuzunguka linaonekana bado ni geni katika vichwa vya wanachi walio wengi, watendaji pamoja na taasisi mbalimbali katika nchi yetu. Na kwa kuwa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kina jukumu kubwa la kutoa elimu kwa wananchi wetu kupitia fani mbali mbali.

Ni lini SUZA itaanzisha Kitivo cha Elimu ya Sayansi ya Mazingira *(Faculty of Environmental Sciences)* kwa tawi la Pemba.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

158. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Katika zama za sasa, kumekuwepo na ukuaji mkubwa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), hali inayochochea kwa kiasi kikubwa uanzishwaji na uendeshaji wa biashara mtandaoni (Online Businesses), kupitia majukwaa mbalimbali ya kidijitali. Biashara hizi zimekuwa na mchango katika uchumi, ajira na ukuaji wa masoko.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kuwa inazitambua rasmi biashara hizi za mtandaoni.

(b) Ni ipi mipango ya Serikali ya kuhakikisha kuwa, wafanyabiashara wanaotumia majukwaa ya kidijitali na mitandao ya kijamii, wanalipa kodi na tozo stahiki.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

223. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Mji Mkongwe wa Zanzibar kwa miaka mingi umekuwa na haiba yake ya kipekee ya kusanyiko la utamaduni mchanganyiko wa watu, majengo, maisha na harakati za uchumi. Hivi sasa haiba na ladha ya utamaduni hiyo inaanza kupotea kwa kuufanya Mji Mkongwe kuwa eneo la utalii tu na ule utamaduni wa watu kuishi unaondoka taratibu kwa watu kuhamishwa au kuhama na kupisha ujenzi wa hoteli, mikahawa na maeneo ya biashara ambayo yameufanya Mji Mkongwe haiba yake iondoke na kubakia jina kama Mfereji wa Wima na Mwembenjugu.

(a) Je, hatari hii ya kupotea haiba ya Mji Mkongwe haionekani na wenye dhamana.

(b) Kwa vile ujenzi wa mahoteli katika Mji Mkongwe umeanza kuwa mkubwa kuzidi idadi ya misikiti na madrasa ambazo zipo toka asili, Je, hali hii haihatarishi sifa ya imani na uchamungu kwa wakaazi wa Mji Mkongwe.

(c) Ikiwa wakaazi wa Mji Mkongwe wanapungua kwa makaazi yao kugeuzwa hoteli za kitalii, Je, misikiti itakayobakia itaswaliwa na nani au nayo itaondoshwa nakugeuzwa vivutio vya utalii.

**<u>Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:</u>**

32. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

    Serikali imeendelea na ujenzi wa miradi ya kujenga barabara za ndani katika visiwa vya Unguja na Pemba. Hata hivyo, katika miradi hiyo zipo baadhi ya kampuni zinaonekana kuelemewa na wingi wa kazi, hali inayosababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wa maeneo ambayo miradi hiyo, imesimama ama kuchukuwa muda mrefu bila ya kukamilika.

    (a) Ni kampuni gani ambazo zimepatiwa kazi ya ujenzi wa miradi ya barabara hizo kwa Unguja na Pemba na kwa thamani ya kiasi gani.

    (b) Ni mkataba wa muda gani ambao Serikali imekubaliana na kampuni hizo, ili kukamilisha miradi yote hiyo hapa Zanzibar.

    (c) Katika mradi huo wa ujenzi wa barabara za ndani, je Serikali ina mpango gani wa kuzijenga na kuzikamilisha kwa haraka barabara ya Mzingani-Wambaa na Kenya- Kwamtora Ukutini.

202. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

    Kasi ya ujenzi wa barabara mpya katika visiwa vya Zanzibar ni jambo la kupongezwa mno. Hata hivyo, baadhi ya barabara zimebaki kwa muda mrefu bila ya kuwekwa taa hali inayopelekea kutokea kwa vitendo vya uhalifu katika baadhi ya mitaa.

    (a) Je, lini ZANROAD itamalizia kuweka taa za barabarani katika Miji ya Zanzibar.

    (b) Je, lini barabara ya Mkoani kuelekea Chake Chake itafungwa taa za barabarani ili kuepusha ajali haswa nyakati za usiku.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

59. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Matumaini ya wananchi wetu wengi yapo katika kilimo ambacho ndio uti wa mgongo wa Taifa letu. Aidha, katika ziara ulizozifanya, nazo zilizidi kuleta matumaini makubwa kwa wananchi hasa wakulima.

(a) Ni changamoto gani ulizozibaini katika ziara zako na katika maeneo gani yanayohusiana na kilimo.

(b) Ni upi mpango wa Serikali katika kutatua changamoto hizo kwa maslahi ya Sekta ya Kilimo.

145. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba inapewa "*Other Charges"* (OC) ndogo sana ukilinganisha na OC za Idara moja ya Wizara hii kwa upande wa Unguja, kitu ambacho kinawarejesha nyuma watumishi wa Wizara, Pemba.

Ni lini Serikali itaondoa ukakasi huu kwenye Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Pemba.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

168. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuboresha Sekta ya Afya kwa kujenga Hospitali za Wilaya, kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi na kupunguza msongamano katika hospitali kubwa. Pamoja na uwepo wa Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake, bado Kituo cha Afya cha Chake Chake kinaendelea kutumika kutoa baadhi ya huduma za afya kwa wananchi bila ya kutoa huduma za uzazi.

(a) Ni lini Serikali itaruhusu Kituo cha Afya cha Chake Chake kutoa huduma za uzazi, ili kupunguza usumbufu na gharama kwa wananchi wa jimbo la Chake Chake.

(b) Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kukifanyia ukarabati kituo hicho, ili huduma zinazotolewa ziwe salama, bora na zenye kukidhi viwango vinavyotakiwa.

170. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na ongezeko la idadi ya wagonjwa wa saratani wanaopatiwa matibabu katika hospitali za Zanzibar na Tanzania bara, hali inayoashiria ukubwa wa changamoto ya ugonjwa huu kwa afya ya jamii na mzigo wa kifedha kwa familia na Serikali.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kitaifa wa kudhibiti na kukabiliana na saratani.

(b) Kwa sasa, Zanzibar ina jumla ya Madaktari Bingwa wangapi wa magonjwa ya saratani.

(c) Je, ni hatua zipi Serikali imepanga au inazotekeleza ili kuimarisha Kliniki za Saratani katika hospitali zetu.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

110. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imeingia ubia na Kampuni ya RAND WATER kwa lengo la kutoa huduma bora zaidi kwa jamii.

(a) Je, ni mafanikio gani yameanza kupatikana katika sekta yetu hii muhimu kwa jamii kupitia Kampuni ya RAND WATER.

(b) Je, ni vifaa vipi vimeletwa na Kampuni ya RAND WATER ili kuongeza ufanisi zaidi.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

71. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ilipanga kununua meli kwa ajili ya uvuvi wa Bahari Kuu kupitia Mradi wa IFAD.

Je, ni meli ngapi zilipangwa kununuliwa na lini meli hizo

zitapokelewa hapa Zanzibar.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

34. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Katika Awamu yake wa Kwanza kwa mwaka 2020-2025, Serikali ya Awamu ya Nane ilitoa ahadi kwa vijana wa kizanzibari ya kutengeneza ajira zipatazo laki tatu (300,000), ahadi ambayo katika Awamu yake ya Pili iliahidiwa kwa ajira laki tatu na hamsini elfu (350,000).

(a) Ni zipi ajira laki tatu (300,000) zilizotengenezwa na Serikali kwa kipindi cha 2020-2025 na ni katika sekta gani ambazo vijana walipata ajira hizo.

(b) Je, ni upi mpango mpya wa Serikali wa kuzitengeneza ajira laki tatu na nusu (350,000) kutoka 2025 hadi 2030 na zitajumuisha sekta zipi.

(c) Ni ipi takwimu na tathmini ya Serikali kuhusiana na Vijana waliomaliza kusoma na kukosa ajira hapa Zanzibar.

## IV. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Tume na Hali ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Nchini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## V. UCHAGUZI WA VIONGOZI WA KLABU YA MICHEZO YA BARAZA LA WAWAKILISHI (BARAZA SPORTS CLUB).

**Zanzibar,**
**25 Februari, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**